ISSN 0856 – 034X

*Supplement No. 14* — *11th April, 2014*

# SUBSIDIARY LEGISLATION

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 15 Vol. 95 dated 11th April, 2014*
Printed by the Government Printer Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 86 la tarehe 11/04/2014

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ( ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI KAHAMA, ZA MWAKA 2014

UTANGULIZI

SEHEMU YA I

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Kahama za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Jina

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Kahama. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kahama.

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Ushuru wa Matangazo" Maana yake ni ushuru machapisho, maandishi, michoro, matamshi ya aina yoyote yanayong'aa na yasiyong'aa yatolewayo na mtu yeyote. kwa madhumuni ya kuufahamisha umma juu ya upatikanaji wa huduma mbalimbali;

"Usajili, wa vyombo vya usaflri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

## SEHEMU YA II

## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa. ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutokana na chanzo husika.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa' kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri Wakala na mlipa Ada na ushuru. .

Uteuzi wa Wakala

6.–(1) Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa;

(a) kukusanya na kupokea ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba;

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba;

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala kwa kila mwezi;

(t) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi; .

## SEHEMU YA III
### Makosa na Adhabu

Makosa na Adhabu

Itakuwa ni kosa kwa:-

7.–(1) kwa wakala;

(a) atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na miwili jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Tangazo la Serikali Na. 86 (linaendelea)*

(2) Kwa yeyote; ..

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na

(f) Atamzuia Afisa Muidhiwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi laki moja (100,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

YAMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (1)

JEDWALI LA KWANZA

I. ADA YA KIBALI CHA SHUGHULI ZA BURUDANI

| Na: | *Aina ya burudani* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | (a) Promosheni za Makampuni ya simu na Kampuni za Biashara zinazoambatana na muziki | Tsh. 500,000/= kwa siku |
| | (b) Tamasha la maonyesho ya urembo | Tsh. 20,000/=.kwa siku |
| | (c) Promosheni za kibiashara za kawaida kwa njia ya vipaza sauti bila muziki | Tsh. 100,000/: kwa siku |
| | (d) Shughuli nyinginezo za kiutamaduni | Tsh. 5,000/= kwa siku |
| 2. | Muziki katika kumbi | Tsh. 50,000/= kwa siku |
| 3. | Michezo ya pool-table | Tsh. 10,000/= kwa mwezi. |

II. ADA YA USAJILI WA TAXI NA PIKIPIKI

| *Na.* | *Aina ya Chombo* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Teksi | Tsh. 24,000/= kwa mwaka |
| 2. | Pikipiki | Tsh. 12,000/= kwa mwaka |

III. ADA NA USHURI WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

| *Na.* | *Chombo cha Usafiri* | *Ushuru wa maegesho* |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria 35 hadi 65 | Tsh. 3,000/= kwa siku |
| 2. | Basi dogo (Costa) la abiria 1 hadi 34 | Tsh. 1,500/= kwa siku |
| 3. | Teksi | Tsh. 500/= kwa siku |
| 4. | Hiace | Tsh. 1 000/= kwa siku |
| 5. | Noa | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 6. | Gari la mtu binafsi lisilo la biashara | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 7. | Pikipiki/daladala | Tsh. 2,000/= kwa siku |

IV. ADA YA MAOMBI YA KIBALI CHA MATANGAZO YA BIASHARA

| Na. | *Aina ya Tangazo* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Tangazo la karatasi-ukubwa A4 | 1,000/= kwa maombi |
| 2. | Tangazo la karatasi-ukubwa wa A3 | 2,000/= kwa maombi |
| 3. | Bango au ubao wa matangazo | 100,000/= kwa mwaka |
| 4. | Bango la Matangazo yaliyoandikwa kwenye kitambaa | 60,000/= Kwa siku |
| 5. | Matangazo ya ukutani/juu ya paa la nyumba | 30,000/= kwa mwaka |
| 6. | Tangazo kwa kutumia vyombo vya usafiri na vipaza sauti | 40,000/= kwa siku |
| 7. | Matangazo kwa kutambulisha bidhaa/huduma katika ofisi za taasisi za umma | 10,000/= kwa siku |

V. ADA NA USHURU WA MAGARI YA MIZIGO

| *Na.* | *Kiwango cha Ushuru* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|
| 1. | Gari la kubeba mizigo lenye Tani 1-3. | Tsh. 1,000/= kwa safari |
| 2. | Gari la kubeba mizigo lenye Tani 4-10 | Tsh. 2,000/= kwa safari |
| 3. | Gari la kubeba mizigo lenye tani 11 na kuendelea | Tsh. 5,000/= kwa safari |

VI. USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO

| *Na.* | *Aina ya Tangazo.* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Tangazo la karatasi-ukubwa wa A4 | Tsh. 1,000/= kwa siku |
| 2. | Tangazo la karatasi-ukubwa wa A3 | Tsh. 2,000/= kwa siku |
| 3. | Tangazo la karatasi -ukubwa zaidi ya A3 | Tsh. 3,000/= kwa siku |
| 4. | Bango la Matangazo yaliyoandikwa kwenye kitambaa | Tsh. 60,000/= kwa siku |
| 5. | Matangazo ya ukutani/juu ya paa la nyumba | Tsh. 4,000/= kwa siku |
| 6. | Ubao wa matangazo unaong'aa | Tsh. 90,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka |
| 7. | Ubao wa matangazo usiong'aa | Tsh 70,000/= kwa mita ya mraba kwa mwaka. |

*Tangazo la Serikali Na. 86 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Matangazo kwa kutumia vyombo vya usafiri na vipaza sauti | Tsh. 50,000/= kwa siku. |
| 9. | Matangazo ya kutambulisha bidhaa/huduma katika ofisi za taasisi au Umma | Tsh. 20,000/= kwa.siku |
| 10. | Bango la tangazo linalobadilikabadilika | Tsh. 200,000/=.kwa mwaka |

VII. ADA YA HUDUMA YA UKUSANYAJI NA OZOAJI WA TAKA

| *Na.* | *Aina ya Biashara* | *Kiwango* |
|---|---|---|
| 1. | Mgahawa mdogo | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |
| 2. | Kioski au Grosali | Tsh. 3,000/= kwa mwezi. |
| 3. | Nyumba ya kulala wageni | Tsh. 5,000/= kwa mwezi. |
| 4. | Zahanati | Tsh. 5,000/= kwa mwezi. |
| 5. | Kituo cha afya | Tsh. 10,000/= kwa mwezi. |
| 6. | Fundi seremala | Tsh. 2,000/= kwa mwezi. |
| 7. | Fundi chuma | Tsh. 20,000/= kwa mwezi. |
| 8. | Karakana au gereji za magari | Tsh. 2,000/= kwa mwezi. |
| 9. | Kiwanda kikubwa | Tsh. 100,000/= kwa mwezi. |
| 10. | Kiwanda kidogo | Tsh. 30,000/= kwa mwezi. |
| 11. | Duka la jumla | Tsh. 30,000/= kwa mwezi. |
| 12. | Duka la rejareja | Tsh. 5,000/= kwa mwezi. |
| 13. | Shule ya msingi ya bweni (za watu binafsi) | Tsh. 15,000/= kwa mwezi. |
| 14. | Shule ya Sekondari ya bweni (za watu binafsi) | Tsh. 30,000/= kwa mwezi. |
| 15. | Duka dogo la vyakula | Tsh. 5,000/= .kwa mwezi. |
| 16. | Duka kubwa la chakula | Tsh. 30,000/= kwa mwezi. |
| 17. | Baa | Tsh. 5,060/= kwa mwezi. |
| 18. | Kumbi za starehe | Tsh. 25,000/= kwa mwezi. |
| 19. | Klabu za usiku | Tsh. 25,000/= kwa mwezi. |
| 20. | Duka la kuuza samaki/nyama | Tsh. 5,000/= kwa mwezi. |
| 21. | Duka la dawa jumla na rejareja | Tsh. 25,000/= kwa mwezi. |
| 22. | Duka la dawa la rejareja | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |
| 23. | Kituo cha mafuta (filling station) | Tsh. 30,000/= kwa mwezi. |
| 24. | Ghala | Tsh.15,000/= kwa mwezi. |
| 25. | Hotel kubwa | Tsh. 15,000/= kwa mwezi |
| 26. | Kiwanda cha mashine ya kukoboa mchele/nafaka | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |
| 27. | Taasisi | Tsh. 20,000/= kwa mwezi |
| 28. | Ofisi za Tasisi kama Benki, Posta, Simu, TANESKO, NSSF | Tsh. 10,000/= kwa mwezi |
| 29. | Stationaries na maduka ya kuuza viatu | Tsh. 5,000/= kwa mwezi. |

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 8)*

Mimi .............................. nakiri mbele ya ................ ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, kwamba mnamo tarehe .............. ya Mwezi ......... Mwaka ............. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha .......... cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Mji wa kahama (Ada na Ushuru) za Mwaka 2013.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe .............................. ya Mwezi .............................. Mwaka...................................

*Jina*.................................................. Saini:.................................................

Mbele ya

Jina:..........................................................................
Cheo:..........................................................................
*Saini* ..........................................................................

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Kahama imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kutokana na Azimio la Mkutano wa Halmashauri. ulioitishwa na kufanyika vilivyo tarehe 05 Mwezi 6 Mwaka 2013 na kubandikwa mbele ya

FELIX H. KIMARYO
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji wa Kahama*

(L.S)

MACHIBYA G. SHIJA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji wa Kahama*

NAKUBALI

Dodoma,
19 Desemba, 2013

MIZENGO P. PINDA (MB)
*Waziri Mkuu.*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 87 la tarehe 11/04/2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA MJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA KAHAMA, ZA MWAKA 201413

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Kahama, 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa muidhinishwa" maana yake ni Afisa Maliasili, Afisa Kilimo na Mifugo na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Eneo la hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kahama.

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na . Afisa muidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote;

"kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti, visiki;

"Maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri;

"maji" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi na maji yaliyoko katika mkondo.

"Maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwanda

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu Na. 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda matete, kamba, makuti mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu.

"Mazingira"kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 yanahusisha maumbile halisi ya wazungukao Binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, viumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mifugo"maana yake ni mnyama yeyote anayefugwa na binadamu;

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asilia au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"Taka" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya , au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira.

"Taka ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwanda na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi, plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo, utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps),

"Taka za viwandani" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa au mawasiliano, pamoja na taka nyingine ngumu kama zilivyotafsiriwa katika sheria ya Mazingira 2004 sehemu IX;

"Uchafu hatari" kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu, chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu, au mazingira;

"Uchafuzi wa Mazingira" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambazo unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi, au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu au kizuizi ambacho ni sehemu katika Sheria Ndogo hizi;

"Udongo" kama ilivyo katika Sheria ya Usimainizi wa Mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni pamoja na mchanga, miamba, tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi;

"Vitu hatari" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ni kemikali yoyote; taka gesi, madawa, vidonge, mimea wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI

### MASHARTI YA UFUGAJI

4.—(1) Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:- Wajibu wa mfugaji

(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoainishwa katika kibali chake kitakachomruhusu kufuga kwa kuzingatia ukubwa wa eneo na kuridhika kwamba ufugaji huo hautakuwa kero kwa majirani.

(b) atatakiwa kufuga ndani ya eneo lake (zero grazing) bila ya kuleta usumbufu kwa jirani zake na jamii kwa ujumla na kuhakikisha sehemu ya kufugia wanyama hao inakuwa safi wakati wote na ana chombo cha kuhifadhi samadi inayotokana na mifugo hiyo.

(c) anayeishi pembezoni mwa Mji atatakiwa kupitisha mifugo, yao katika njia zilizopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri

(f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote;. Masharti ya mfugaji

(a) kuchunga kulisha na kunywesha maji mifugo katika maeneo ya mipango miji pamoja na maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi jingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;

(d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;

(e) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;

(f) Ni marufuku kwa mfugaji yeyote kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo;

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

6.—(1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo;

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama ilivyooneshwa kwenye jedwali na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au, mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au, mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea kufa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

Ukaguzi wa mifugo

7.—(1) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo na Mifugo, Maafisa watendaji wa Kata na Vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8.—(1) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalum. kwa ajili ya shughuli za malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

(2) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi ya mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9.–(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia nyama mahali pengine popote.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada ya magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

## SEHEMU YA TATU

### KILIMO NA HIFADHI YA ARDHI .

Taratibu za kilimo

10.–(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.

(2) Itakuwa halali kwa Afisa Kilimo kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mkulima

11.–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo Michango ya jamii.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko (crops roration).

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira, ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya barabara, mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa katikati ya barabara.

14. Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

## SEHEMU YA NNE
### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15.—(1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Maeneo yaliyotajwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi, yamehifadhiwa.

(3) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

Kulinda eneo lahifadhi

16.—(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kufuga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa kwa ruhusa ya Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17.—(1) Ni marufuku mtu yeyote, kiwanda, taasisi, shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

## SEHEMU YA TANO

### HIFADHI YA MISITU

18.—(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri. Kuchoma au kusababisha moto

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo. endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

19. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma mota atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma, moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto. Kibali cha kuchoma moto

20.—(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri. Ukataji miti

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

21. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika;- Wajibu wa kupanda miti

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake.

(b) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji;

(a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya misitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadae;

(b) kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;

(c) kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake;

(d) mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi yakuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, inabidi apate kibali cha maandishi toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa Wilaya au wasaidizi wake kwa miti iliyopanda na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya;

(e) kinapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza;

(f) kila shule au taasisi nyingineyo katika Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka, majengo yake;

(g) Mitaa/Kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;

(h) Kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;

(i) Kila mtu mwenye nyumba kwenye eneo la kati ya Mji atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza;

(j) Kila Mwenyekiti wa Mtaa, Mtendaji wa kijiji, Mkuu wa taasisi yoyote atahakikisha kuwa ina msitu wahifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA

### HIFADHI (MAKABURI)

23.—(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo ya makaburi na kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa katika hali ya usafi ha usalama.

(2) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuzika mwili wa binadamu katika maeneo ambayo hayakutengwa na Hamashauri ya Mji au Vijiji.

(3) Iwapo mtu yeyote atataka, kuzika eneo tofauti na lililotengwa atapaswa kuomba kibali kutoka Halmashauri ya Mji.

## SEHEMU YA SABA

### TAKA NGUMU NA LAINI

24. (1) Niwajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini au kujisaidia/ kuoga katika kingo za maziwa, mabwawa, mito au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa

25. Ni marufuku kuendesha, shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta. athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi. Uendeshaji wa viwanda

SEHEMU YA NANE

MAKOSA NA ADHABU

26. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa: . Makosa yanayohusu mifugo

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali;

(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa;

(e) atavua samaki kwa kutumia; sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro)

27. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa. Makosa yanayohusu kilimo

28. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi ardhi atakuwa ametenda kosa. Makosa yanayohusu kuhifadhi ardhi

29.–(1) Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa. Makosa yanayohusu vyanzo vya maji

(2) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

30. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa: Makosa yanayohusu kuharibu misitu

(a) atachoma au kusababisha moto katika msitu bila kibali, au

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto, au .

(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa isiyohifadhiwa bila kibali; au

(d) atachoma mkaa na kukata kuni, bila kibali; au .

(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye eneo bila kibali; au

(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa. miti iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;

(g) atakata miti, au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa. kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo.

(h) atabandua magome ya miti kwa ajili. ya kutengeza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali.

(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

31. Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika eneo lolote lisiloruhusiwa na atakuwa ametenda kosa kutokana na Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

32. Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu viwanda

33. Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa

34. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

adhabu

35. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa Kahama imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi zilibandikwa kufuatia azimio la kikao cha Halmashauri yamji wa Kahama kilichoketi vilivyo na kufanyika tarehe 05 mwezi 06 mwaka 2013 Lakiri hiyo lilibandikwa mbele ya:-

FELIX H. KIMARYO
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji Kahama.*

(L.S)

MACHIBYA G. SHIJA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji Kahama.*

NAKUBALI,

Dodoma
19 Desemba, 2013

MIZENGO .P. PINDA (MB)
*Waziri Mkuu.*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 88 la tarehe 11/04/2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO ZA (MATUMIZI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MJI KAHAMA, ZA MWAKA 2013

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Matumizi ya Barabara) za Halmashauri ya Mji wa Kahama za mwaka 2014 zitaaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote la Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Eneo la kati" maana yake ni eneo la kata ya Shangani.

"Gari" maana yake ni chombo chochote kile cha moto chenye matairi kuanzia matatu.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kahama.

"Kituo"maana yake ni kituo kilichosajiliwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha teksi, pikipiki, gari, na lori.

"Kituo cha teksi" maana yake ni kituo maalum kilichoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha teksi.

"Kituo cha Basi" maana yake ni Kituo maalum kilichoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha mabasi yanayoshusha na kupakia abiria.

"Lori" maana yake ni gari yoyote ile ya mzigo yenye uzito kuanzia tani $3\frac{1}{2}$ na kuendelea.

"Maegesho" maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya kuegesha magari.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mtaa" maana yake ni eneo lolote ndani ya Halmashauri na inajumuisha barabara.

"Mkokoteni" maana yake ni chombo chochote kile chenye matairi kinachotumika kubeba mizigo ambacho hutembea kwa kusukumwa na binadamu au kukokotwa na mnyama.

"Teksi" maana yake ni gari yeyote iliyosajiliwa yenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi watano inayotumika kufanya biashara ya kusafirisha watu, ikiwa ni pamoja na bajaji na pikipiki.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au Shirika atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kwa niaba yake.

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Maegesho

4.–(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari sehemu yoyote isipokuwa katika eneo lililotengwa maalum kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola itahakikisha inaweka alama za barabarani zitakazoonyesha sehemu maalum kwa ajili ya kuegesha magari katika Mitaa yote ndani ya Halmashauri.

Usajili wa teksi

5.–(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa teksi kuhakikisha kwamba:-

(a) gari lake limekaguliwa na Polisi na amelipia kodi zote zinazotakiwa na Serikali ikiwa ni pamoja na Kodi, Ada na Ushuru wa Halmashauri kabla ya kusajiliwa.

(b) teksi yake imesajiliwa na Halmashauri kabla ya kuanza kufanya biashara ya kusafirisha abiria.

(2) Baada ya kusajiliwa, Halmashauri itatoa namba itakayobandikwa ubavuni mwa gari na kuainisha kituo ambacho teksi iliyosajiliwa itaegeshwa.

Usajili wa vituo Vya teksi

6.–(1) Halmashauri itatenga na kutangaza maeneo maalum yatakayotumika kama vituo vya teksi.

(2) Halmashauri itaainisha idadi ya teksi zitakazoruhusiwa kuegeshwa katika kituo kimoja kwa wakati mmoja kwa kuzingatia ukubwa wa eneo.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha teksi mahali ambapo hapakutengwa kwa ajili ya matumizi hayo.

Mikokoteni

7.–(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa mkokoteni kuusajili mkokoteni wake kwenye Kata anayofanyia biashara ya kuendesha Mkokoteni.

Malori

(2) Baada ya kusajiliwa Afisa Mtendaji wa Kata ataupatia mkokoteni huo namba na kuupangia eneo ambalo utatakiwa kuegeshwa.

(3) Kila mkokoteni utalipiwa ada ya usajili kama itakavyopangwa na Halmashauri.

8.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa lori lolote kuingia eneo la kamati la Halmashauri bila kupata kibali cha Maandishi cha Halmashauri.

(2) Eneo la kati la Biashara la Wilaya (Central Business District) kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na Kata ya Mjini, Ibinzamata, Lubaga, Kambarage, Ngokolo Ndala, Kitangili, Ndabezi na eneo lingine lolote ambalo Halmashauri itaamua kufanya hivyo.

(3) Kibali cha kuingiza lori eneo la kati kita lipiwa ada ya shilingi 30,000/= kwa kila safari Halmashauri inaweza kubadili kiwango endapo itaona inafaa kufanya hivyo.

(4) Kibali kilichotolewa kitatumika kwa safari moja na kwa siku iliyotajwa kwenye kibali kwa kupitia barabara zile tu zitakazoainishwa ndani ya kibali hicho.

(5) Kibali cha kuingiza lori eneo la kati la Halmashauri kitatolewa na Halmashauri baada ya kupokea maombi ya maandishi kutoka kwa muombaji akiainisha lengo la kuingiza lori eneo la kati na mahali linapokwenda.

Uoshaji na utengenezaji wa magarl

9.—(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha na au kutengeneza gari katika eneo la barabara, hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo halijatengwa kwa matumizi hayo.

(2) Gari litalokutwa linaoshwa au kutengenezwa katika maeneo yasiyoruhusiwa litavutwa na kupelekwa katika Ofisi za Halmashauri na mmiliki wa gari hilo atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=).

(3) Pamoja na faini iliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) mmiliki wa gari lililovutwa atatakiwa pia kulipa shilingi elfu arobaini (40,000/=) ikiwa ni gharama za kuvuta gari, na shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) kwa siku ikiwa ni gharama ya kutunza gari hilo, iwapo litatunzwa kwenye eneo la Halmashauri au kiwango cha gharama kitakachobainishwa na mmiliki wa eneo la kuhifadhia gari.

(4) Iwapo gari lililokamatwa litakaa katika ofisi za Halmashauri kwa zaidi ya siku kumi na nne (14) Halmashauri itauza gari hilo kwa mnada baada ya kuomba na kupata kibali cha mahakama ili kufidia gharama zake na kiasi cha fedha kitakachobaki atarudishiwa mmiliki wa gari.

Ufungaji wa barabara

10.—(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufunga barabara kwa ajili ya sherehe, msiba au shughuli nyingine yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri. Kibali cha kufunga barabara kwa siku kitalipiwa shilingi laki moja (100,000/=) .

(2) Mtu yeyote ambaye atafunga barabara bila idhini ya Halmashauri atakua ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatotwa faini isiyozidi shillingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela au vyote viwili yaani faini na kifungo.

Uwekaji wa vifaa vya ujenzi barabarani

11. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kama kokoto, mchanga, mawe na vifaa vinginevyo vya ujenzi katika eneo la hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhusiwa bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

Kukata barabara

12.—(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukata barabara kwa ajili ya kupitisha mabomba ya maji, nyaya za umeme, simu au shughuli nyingine yoyote ile bila ya kuwa na kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayetaka kukata barabara kwa ajili ya kupitisha miundo mbinu mingine atatakiwa kulipa ada ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa barabara ya lami, Shilingi elfu arobaini (40,000/=) kwa kila mita ya urefu, kwa barabara za changarawe shilingi elfu ishirini (20,000/=) na atatakiwa kurejesha barabara inayohusika kwenye hali yake ya awali kwa muda utakaotengwa na Halmashauri.

(3) Kibali cha kukata barabara kitadumu kwa muda wa siku saba (7) tu, na baada ya hapo tozo la faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) itatozwa kila siku ambayo muombaji atashindwa kurekebisha eneo lililokatwa na kurejesha barabara katika hali yake ya awali.

Barabara na uzito wa magari

13.—(1) Kila barabara itakua na uzito wa magari yanayoruhusiwa kupitisha katika barabara hiyo. Halmashauri itaweka katika kila barabara bango linaloonyesha uzito wa gari wa magari yanayoruhusiwa kupitishwa katika barabara hiyo.

(2) Hakuna gari lolote litakaloruhusiwa kupitishwa katika barabara yoyote iwapo uzito wa gari hilo utakuwa mkubwa kuliko uzito wa magari yaliyoruhusiwa kupitishwa katika barabara hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayepitisha gari katika barabara yoyote kinyume na Kifungu cha 15(2) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi elfu hamsini(50,000/=) pamoja na gharama za uharibifu wa barabara zilizothaminiwa na Halmashauri au kifungo kisichozidi miezi sita jela au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Ujenzi kwenye eneo la Barabara

13.–(1) Mtu yeyote ambaye atakua amejenga au ameweka jengo lolote katika, eneo la barabara mara baada ya Sheria Ndogo hii kuanza atatakiwa kupewa notisi ya siku kumi na nne.

(2) Iwapo baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne mtu huyo ameshindwa kutekeleza amri hiyo Halmashauri itabomoa na kumpelekea gharama za ubomoaji huo mhusika.

Uzibuaji wa mitaro

14.–(1) Pale ambapo njia ya kuingilia kwenye nyumba imejengwa kwa namna ambayo inaweza kuziba mitaro iliyo kwenye barabara na kuzuia mtiririko wa maji kwenye mitaro hiyo Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa anaweza kumtumia notisi mtu anayemiliki jengo hilo aweke culvert au bomba eneo hilo kama itakavyoelezwa kwenye notisi hiyo kwa lengo la kuondoa tatizo la uzibaji wa mitaro husika.

(2) Endapo kuna njia ya kuingia kwenye makazi na pamewekewa culvert au bomba mwenye jengo husika au makazi kwenye jengo hilo atatakiwa kuliacha wazi eneo hilo bila kuliziba na kuzuia maji kupita na atahakikisha eneo hilo liko kwenye hali nzuri na endapo atakiuka masharti ya fungu hili, Halmashauri itafanya kazi hiyo na kisha kumtaka mhusika alipie gharama ambazo Halmashauri itakua imetumia.

(3) Itakua ni jukumu la mwenye nyumba kuhakikisha mtaro unaozunguka au uliopo mbele ya nyumba au jengo lake la biashara unakua katika hali ya usafi wakati wote.

Majengo yanayojitokeza

15. Hairuhusiwi kwa mtu yoyote, bila kupata kibali maalum kutoka Halmashauri, kujenga, kuning'iniza au kuweka jengo lolote au kusababisha jengo kuingia katika eneo la barabara.

kufanya biashara

16.–(1) Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kufanya biashara katika eneo la barabara.

(2) Hakuna gari lolote litakaloruhusiwa kupitishwa katika barabara yoyote iwapo uzito wa gari hilo utakuwa mkubwa kuliko uzito wa magari yaliyoruhusiwa kupitishwa katika barabara hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayepitisha gari katika barabara yoyote kinyume na Kifungu cha 15(2) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi elfu hamsini(50,000/=) pamoja na gharama za uharibifu wa barabara zilizothaminiwa na Halmashauri au kifungo kisichozidi miezi sita jela au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Ujenzi kwenye eneo la Barabara

13.—(1) Mtu yeyote ambaye atakua amejenga au ameweka jengo lolote katika, eneo la barabara mara baada ya Sheria Ndogo hii kuanza atatakiwa kupewa notisi ya siku kumi na nne.

(2) Iwapo baada ya kupewa notisi ya siku kumi na nne mtu huyo ameshindwa kutekeleza amri hiyo Halmashauri itabomoa na kumpelekea gharama za ubomoaji huo mhusika.

Uzibuaji wa mitaro

14.—(1) Pale ambapo njia ya kuingilia kwenye nyumba imejengwa kwa namna ambayo inaweza kuziba mitaro iliyo kwenye barabara na kuzuia mtiririko wa maji kwenye mitaro hiyo Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa anaweza kumtumia notisi mtu anayemiliki jengo hilo aweke culvert au bomba eneo hilo kama itakavyoelezwa kwenye notisi hiyo kwa lengo la kuondoa tatizo la uzibaji wa mitaro husika.

(2) Endapo kuna njia ya kuingia kwenye makazi na pamewekewa culvert au bomba mwenye jengo husika au makazi kwenye jengo hilo atatakiwa kuliacha wazi eneo hilo bila kuliziba na kuzuia maji kupita na atahakikisha eneo hilo liko kwenye hali nzuri na endapo atakiuka masharti ya fungu hili, Halmashauri itafanya kazi hiyo na kisha kumtaka mhusika alipie gharama ambazo Halmashauri itakua imetumia.

(3) Itakua ni jukumu la mwenye nyumba kuhakikisha mtaro unaozunguka au uliopo mbele ya nyumba au jengo lake la biashara unakua katika hali ya usafi wakati wote.

Majengo yanayoji-tokeza

15. Hairuhusiwi kwa mtu yoyote, bila kupata kibali maalum kutoka Halmashauri, kujenga, kuning'iniza au kuweka jengo lolote au kusababisha jengo kuingia katika eneo la barabara.

kufanya biashara

16.—(1) Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kufanya biashara katika eneo la barabara.

(2) Iwapo Halmashauri itagundua mtu yoyote ameweka bidhaa zake katika eneo la hifadhi ya barabara mtu huyo atapewa notisi ya siku kumi na nne ili kuondoa bidhaa zake na asipofanya hivyo Halmashauri itaondoa bidhaa hizo na kumtaka alipe gharama za uondoaji wa bidhaa hizo.

13. Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumteua Wakala kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kwa niaba yake. Uteuzi wa wakala

14. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo:- Makosa

(a) ataegesha gari katika sehemu isiyoruhusiwa;

(b) atafanya biashara ya teksi kwa kutumia gari isiyosajiliwa au kuegesha kwenye kituo cha teksi;

(c) ataendesha mkokoteni bila ya kusajili katika Kata;

(d) ataendesha mkokoteni katika barabara ambayo hajaruhusiwa;

(e) ataendesha lori bila kibali katika eneo la kati la Halmashauri

(f) ataosha gari katika eneo la barabara hifadhi ya barabara au eneo la wazi ambalo matumizi yake siyo ya kuegesha gari;

(g) atafunga barabara kwa shughuli za sherehe msiba au shughuli nyingine yoyote bila kibali cha maandishi cha Halmashauri;.

(h) atakata barabara bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri.

(i) ataweka au kumwaga vifaa vya ujenzi kwenye barabara, hifadhi ya barabara au eneo lisiloruhusiwa.

(j) atamzuia Afisa au Wakala wa Halmashauri kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

15. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi mitatu Jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo. Adhabu

16. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa. Kufifilisha kosa

JEDWALI LA PILI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi)*

Mimi.......................................................................wa SLB...................................... ninaefanya biashara ya.................................................. katika eneo la........................................................ lililopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Kahama.
Nakiri kuwa leo tarehe...........................................................................Nilikiuka kifungu cha ...................................................................cha Sheria Ndogo za (Matumizi ya Barabara) za Halmashauri ya Mji wa Kahama za mwaka, 2013. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini.........................................................................................

Mbele yangu.............................................................................(jina)

Saini.........................................................................................

Wadhifa.....................................................................................

Lakiri na Mhuri wa Halmashauri ya Mji wa Kahama ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Kikao cha Halmashauri ya Mji wa Kahama kilichofanyika tarehe 05 mwezi 06 mwaka 2013 na ulibandikwa mbele ya :

Felix H. Kimaryo
*Kaimu Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Mji wa Kahama.*

L.S

Machibya G. Shija
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji wa Kahama*

NAKUBALI

Dodoma
19 Desemba, 2013

Mizengo P. Pinda (Mb)
*Waziri Mkuu.*

ISSN 0856 – 034X

*Supplement No. 14* *11th April, 2014*

# *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 15 Vol. 95 dated 11th April, 2014*
Printed by the Government Printer Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 89 la tarehe 11/04/2014

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu vya 6(3) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ( KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MJI WA KAHAMA, ZA MWAKA 2014

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Mji wa Mji wa Kahama za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Mji wa Kahama.

Tafsiri

3.Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhiniwa" Maana yake ni mtu au Afisa yeyote aliyeruhusiwa na Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

"Ghala" Maana yake ni jengo au nyumba inayotumika kwa matumizi ya kuhifadhia vitu mbalimbali.

"Ghorofa" Maana yake ni jengo lenye ghorofa zaidi ya moja.

"Halmashauri" Maana yake Halmashauri ya Mji wa Kahama na eneo lake la kiutawala. .

"Jengo" Maana yake ni nyumba au jengo lolote linalotumika kwa ajili makazi ya mtu/watu au nyumba au jengo lolote linalotumika kwa shughuli za kibiashara tu pia inajumuisha nyumba inayotumika kwa shughuli za makazi na biashara kwa pamoja.

"Kiwanda" Maana yake ni jengo linalotumika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa ukarabati au ukarafati wa vitu mbalimbali.

"Mali" Maana yake ni kiwanja, jengo, nyumba na inajumuisha uendeshaji wa nyumba au jengo kwa umbo lake.

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mji wa Kahama.

"Ushuru" Maana yake ni ushuru wa mali unaotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Usajili

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa jengo ndani ya eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba jengo lake limesajiliwa na Halmashauri, na kupewa namba maalumu ya utambuzi ya mlipa Kodi ya Majengo na namba hiyo ibandikwe sehemu ya wazi inayoonekana.

Wajibu wa mmiliki

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki ambaye anamiliki jengo ndani ya Halmashauri:-

(a) kulipa kodi ya majengo kama ilivyoelekezwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(b) kuhakikisha kuwa jengo lake limesajiiiwa na kuingizwa kwenye orodha ya walipa kodi.

Muda wa kulipa kodi

6.—(1) Kodi ya Majengo itozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kwa Halmashauri au Wakala wake kuanzia tarehe 1 Julai na mwisho wa malipo hayo itakua kila au kabla ya tarehe 30 ya mwezi wa Machi ya kila mwaka.

(2) Baada ya tarehe iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu, kila mmiliki wa mali ambaye atakuwa hajalipa ushuru huo, atalazimika kulipa ushuru pamoja na faini ya asilimia hamsini (25%) ya deni lote.

(3) Baada ya tarehe thelathini na moja ya mwezi Machi ya kila mwaka, endapo mtu huyo atashindwa kulipa kodi baada ya muda wa notisi ya siku kumi na nne (14) kupita, Halmashauri itaomba Mahakama yenye mamlaka amri ya kukamata au kushikilia mali ya mdaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Msamaha wa kodi

7. Halmashauri inaweza kupunguza au kufuta kabisa Kodi ya Jengo kwa majengo yaliyoorodheshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala

8.—(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa wakala

(2) Wakala aliyeteuliwa kukusanya kodi ya majengo atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya na kupokea Kodi kutoka kwa kila mmiliki ambaye anawajibika kulipa Kodi ya Majengo na kuwasilisha malipo hayo Halmashauri kwa tarehe na utaratibu utakaokuwa umeainishwa kwenye mkataba.

(b) kutoa taarifa kwa Halmashauri jina la mtu aliyeshindwa au kukataa kulipa Kodi.

(3) Wakala yeyote ambaye:- Makosa ya wakala

(a) atashindwa kuwasilisha Halmashauri kiasi cha Kodi alichokusanya;

(b) kwa makusudi atadai kutoka kwa mmiliki yeyote kiasi cha fedha kuzidi alichotakiwa. kutozwa;

(c) kwa makusudi atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) atashindwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kama Mkusanya Kodi chini ya Sheria Ndogo hizi.

atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo pamoja kulipa hasara atakayokuwa ameisababishia Halmashauri.

9. Mmiliki yeyote ambaye atakataa au kushindwa kulipa Kodi ya Majengo au kushindwa kusajili jengo lake atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo pamoja na hasara atakayokuwa ameisababishia Halmashauri. Makosa na adhabu

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa. Kufifilisha kosa

*Tangazo la Serikali Na. 89 (linaendelea)*

JEDWALI LA KWANZA

A

| S/Na. | Aina ya kiwanja /nyumba/jengo | Matumizi ya mali | Kiasi |
|---|---|---|---|
| | A. Viwanja | | |
| 1. | Eneo dogo (Ujazo Mdogo) | i. Makazi<br>ii. Biashara<br>iii. Makazi ya biashara | 5,000/=<br>10,000/=<br>15,000/= |
| 2. | Eneo la kati(Ujazo wa Kati) | i. Makazi<br>ii. Biashara<br>iii. Makazi ya biashara | 10,000/=<br>15,000/=<br>20,000/= |
| 3. | Eneo kubwa (Ujazo Mkubwa) | i. Makazi<br>ii. Biashara<br>iii. Makazi ya biashara | 20,000/=<br>25,000/=<br>25,000/= |
| 4. | Kiwanda | i. matumizi ya viwanda | 400,000/= |
| 5. | Ghala | i. Biashara/makazi | 200,000/= |
| 6. | Nyumba kubwa | i. Biashara | 50,000/= |
| 7. | Nyumba kubwa | i. Biashara na makazi | 80,000/= |
| 8. | Ghorofa | i. Bishara<br>ii. Makazi | 100,000/=<br>100,000/= |

JEDWALI LA PILI

FOMU YA SUMMARY WARRANT YA KUSHIKA NA KUUZA

Kwa Dalali wa Mahakama

*(Chini ya kifungu cha 6 (3) cha Sheria Ndogo hizi)*

Hivi ni kukuamuru kukamata mali inayohamishika ya ..............................................kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo juu atalipa kiasi cha shilingi ................................ ikiwa ni ushuru unaodaiwa na Halmashauri ya Mji pamoja na riba ya kiasi cha shillingi............................. kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi kutoka tarehe ..........................ya mwezi ................... mwaka................................

Na gharama za ukamataji huu na baada ya kumpatia kusudio la siku kumi na nne (14) na kuitarifu Mahakama muda huo na baada ya kufanya madai halali ya kuuza kwa mnada mali au sehemu ya mali itakayokidhi thamani ya shilingi ......................................kama ilivyofafanuliwa hapo juu.

Na unaamriwa tena kurudisha fomu hii siku au kabla ya siku ya ................................ ya mwezi wa ................................ ya mwaka ................................ ikiwa imesainiwa kuthibitisha jinsi ilivyotelekezwa au sababu za kutotekeleza.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama leo.....................siku ya ...............mwezi ..................wa mwaka..........................